



# Fursa na Haki za Wanawake Kiuchumi Tanzania

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

WiLDAF

**SHIRIKA LA WANAWAKE KATIKA SHERIA NA MAENDELEO BARANI AFRIKA (WiLDAF)**

Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 1 1/3/2017 10:32:46 AM

# Fursa na Haki za Wanawake Kiuchumi Tanzania

Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 3 1/3/2017 10:32:46 AM

Kitabu hiki kimeandaliwa na kuchapishwa na:

Women in Law & Development in Africa

SHIRIKA LA WANAWAKE KATIKA SHERIA NA MAENDELEO BARANI AFRIKA
(WiLDAF)
Mikocheni "A" Mtaa wa Chwaku Kitalu F, Kiwanja Na. 635
SLP 76215 Dar es Salaam, Tanzania.
Simu:+255 22 270 1995
wildaf_tanzania@yahoo.com
info@wildaftanzania.org

www.wildaftanzania.org

Mwandishi: Utti Mwang'amba

© WiLDAF Tanzania, 2016

ISBN: 978 - 9987 - 9246 - 9 1

Usanifu: Marco Tibasima

Kitabu hiki kimetolewa kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID). Hata hivyo yaliyomo kwenye kitabu hiki siyo lazima yawakilishe maoni na mitazamo ya mfadhili. WiLDAF inawajibika kwa mapungufu yoyote yatakayojitokeza katika kitabu hiki.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 4 1/3/2017 10:32:46 AM

# KUHUSU SHIRIKA LA WiLDAF

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), ni mtandao wa mashirika na watu binafsi katika bara la Afrika ambao unafanya kazi za kupigania haki za wanawake, kujitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo ili kuongeza ushiriki na ushawishi wa wanawake katika mikakati na pia kueneza chachu hiyo katika ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa.

WiLDAF ilisajiliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1997 chini ya sheria ya Makampuni sura ya 212 kama Shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kisiasa na lisilojiendesha kwa faida.

WiLDAF Tanzania ina maono ya kuwa na jamii ya Tanzania inayoheshimu haki za binadamu za wanawake. Na Dhima yake ni kujenga mtandao imara wa vyombo mbali mbali vya kitaifa na kimataifa pamoja na mpango wa dharura wa kuitikia ukatili wa kijinsia katika ngazi zote wakati huo huo ikihusisha sheria na maendeleo.

# SHUKRANI

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika, Tawi la Tanzania (WiLDAF Tanzania) linatoa shukrani za dhati kwa mbia wetu wa maendeleo Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) Kwa kudhamini utayarishaji, uchapaji na usambazaji wa kitabu hiki. Kwa upendo mkubwa elimu hii itaweza kuifikia jamii pana ya watanzania na kuwafanya baadhi yao hasa wanawake kuwa ni sehemu ya kuzisimamia haki zao kiuchumi na vilevile kuzitumia fursa zilizopo katika kuleta maendeleo kiuchumi kwa mwanamke na jamii kwa ujumla wake.

Shirika la WiLDAF Tanzania linawashukuru wafanyakazi wake Bi. Anna Kulaya na Dr. Judith Odunga kwa kuandaa rasimu ya kwanza ya kazi hii. Shukrani za dhati ziyafikie mashirika mbali mbali ambayo ni wanachama wa WiLDAF kwa kutoa maoni yao kwa njia mbali mbali.

Shukrani za dhati kwa wakili Utti Mwang'amba kwa kuandaa na kupitia kitabu hiki.

Shirika la WiLDAF pia linawashukuru wadau wafuatao walioshiriki katika semina ya mapitio ya kitabu hiki na kutoa michango yao kwa ajili ya kuboresha kitabu hiki;

| | | |
|---|---|---|
| 1. Catherine Tenga | - | Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MOHCDEC) |
| 2. Japhace Daudi | - | Law Reform Commission (LRC) |
| 3. Christina Onyango | - | Tanzania Police Female Network (TPFNET) |
| 4. Mackphason Buberwa | - | Tanganyika Law Society (TLS) |
| 5. Jovin Sanga | - | Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA) |
| 6. Faudhia Yasin | - | Women's Legal Aid Centre (WLAC) |
| 7. Edda Maliki | - | Tanzania Women and Children Welfare Centre (TWCWC) |
| 8. Gloria Misana | - | Tanzania Children and Women Welfare Centre (TWCWC) |
| 9. Fransisca Silayo | - | Child Dignity Forum |
| 10. Neema Duma | - | Women Fighting HIV/AIDS in Tanzania (WOFATA) |
| 11. Bankunda Bitwale | - | Women in Law and Development in Africa (WiLDAF) |
| 12. Jacquiline Waya | - | Women in Law and Development in Africa (WiLDAF) |
| 13. Neema Mayunga | - | Women in Law and Development in Africa (WiLDAF) |
| 14. Anna Kulaya | - | Women in Law and Development in Africa (WiLDAF) |




Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 6 1/3/2017 10:32:46 AM

# YALIYOMO

KUHUSU SHIRIKA LA WiLDAF ....................iii
SHUKRANI ....................iv
YALIYOMO ....................v
USULI ....................vii
VIFUPISHO ....................ix
UTANGULIZI ....................x
Ufafanuzi wa Istilahi ....................xi

**SEHEMU YA KWANZA** ....................1
1.0 MIKATABA YA KIMATAIFA YA HAKI ZA WANAWAKE KIUCHUMI....................1
1.1 MIKATABA YA KIMATAIFA .................... 1

**SEHEMU YA PILI** ....................6
2.0 SERA, MIPANGO, MIKAKATI NA SHERIA ZA TAIFA ZINAZOLINDA NA KUINUA UCHUMI WA WANAWAKE ....................6
2.1 SERA ZA KITAIFA ZINAZOLENGA KUINUA UCHUMI WA WANAWAKE ....................6
2.2 MIPANGO YA TAIFA .................... 7
2.3. SHERIA NA HAKI ZINAZOLINDA NA KUINUA UCHUMI KWA WANAWAKE ....................8

**SEHEMU YA TATU** ....................18
3.0. SHERIA ZINAZOATHIRI FURSA ZA WANAWAKE KIUCHUMI ....................18
3.1 SHERIA YA KIMILA YA MWAKA 1963 -TANGAZO LA SERIKALI NA.436 /1963 ....................18
3.2. SHERIA YA NDOA YA MWAKA 1971....................19

**SURA YA NNE** ....................20
4.0. TAASISI ZA KIFEDHA NA MFUKO WA WANAWAKE KATIKA KUKUZA UCHUMI ....................20
4.1. BENKI YA WANAWAKE ....................20
4.2. HUDUMA ZA BENKI NYINGINE ....................20
4.3. MFUKO WA WANAWAKE KATIKA KUKUZA UCHUMI (WDF).................... 21
4.4. BENKI ZA KIJAMII NA TAASISI NDOGO NDOGO ZA FEDHA ....................21
4.5. SACCOS .................... 24
4.6. FURSA YA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI ....................26



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 7 1/3/2017 10:32:47 AM

**SEHEMU YA TANO** ............................................................28
5.0. HATUA ZA KUJENGA JAMII ISIYOKUWA NA UKATILI WA KIUCHUMI ............................................................28
5.1. MABORESHO YA KISERA NA KISHERIA ............................................28
5.2. UHAMASISHAJI JAMII ............................................................29
5.3. WADAU WA MAENDELEO ............................................................29
5.4. UTAFITI............................................................30

**HITIMISHO**............................................................ 30

**VIAMBATANISHO**............................................................ 31

# USULI

Kitabu hiki kinaelezea haki na fursa mbali mbali zilizopo kwa wanawake ili waweze kujiinua kiuchumi na pia aweze kuepukana na ukatili wa kiuchumi. Kitabu hiki kinatoa mwanga siyo tu kwa wanawake bali pia kwa wanaume ili waweze kufahamu na kuelewa kuwa wanawake wana haki na fursa sawa za kumiliki na kutumia rasilimali zilizopo katika kuinua uchumi binafsi na wa jamii yake kwa ujumla.

Kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu kuu tano ambazo zinanyumbulishwa kama ifuatavyo;

**Sehemu ya Kwanza**: Inaelezea Mikataba ya Kimataifa na Sheria mbali mbali zinazoelezea haki ya uchumi kwa wanawake.

**Sehemu ya Pili**: Sera, Mipango, Mikakati na Sheria za Nchi zinazolinda na kuinua uchumi wa wanawake. Sehemu hii inaelezea Wajibu wa Serikali katika kuinua Haki za Kiuchumi.

Pia sehemu hii inaelezea sera zilizopo katika kuwakomboa wanawake kiuchumi, mikakati na sheria zilizopo katika kuhakikisha wanawake wanapata fursa na haki za kiuchumi.

**Sehemu ya Tatu**: Inaelezea upungufu wa Sheria na utekelezaji katika kuondoa ukatili wa kiuchumi ambapo maelezo ya kutosha juu ya mapungufu yaliyopo kwenye sheria na utekelezaji wake yamechambuliwa ili kumpa msomaji mwanga na uwezo wa kuchambua na kuona ni jinsi gani ya kufanya utetezi juu ya sera na sheria hizi ili ziweze kuendana na wakati uliopo na ziweze kutoa fursa na haki sawa kwa wanawake na wanaume.

**Sehemu ya Nne:** Inaelezea Taasisi za Kifedha na Mfuko wa Wanawake katika kukuza uchumi.

**Sehemu ya Tano:** Kitabu hiki kinatoa hatua za kujenga jamii isiyokuwa na ukatili wa Kiuchumi ikiwa ni pamoja na maboresho ya kisera na kisheria, uhamasishaji wa jamii na wadau wa maendeleo pamoja kufanya tafiti. Hii itaisaidia serikali katika kutengeneza sera, sheria na mipango inayohamasisha upatikanaji wa fursa na haki kwa wanawake.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 9 1/3/2017 10:32:47 AM

Mwisho kabisa kitabu hiki kinatoa hitimisho ambalo shirika la WiLDAF linaamini kitabu hiki kwa ujumla kitakuwa kimetoa mwanga na njia kwa wanawake na wanaume kuzifuata ili waweze kutumia kwa usahihi fursa zilizopo katika kufikia haki zao kiuchumi.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 10 1/3/2017 10:32:47 AM

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| EWURA | - | Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati, Maji na Mafuta |
| VICOBA | - | Benki ya Jamii Vijijini |
| CEDAW | - | Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake |
| SACCOS | - | Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo |
| CRDB | - | Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini |
| NBC | - | Benki ya Taifa ya Biashara |
| TIB | - | Benki ya Rasilimali Tanzania |
| WDF | - | Mfuko wa Wanawake katika kukuza uchumi |
| TFDA | - | Mamlaka ya Chakula na Dawa |
| TPB | - | Benki ya Posta Tanzania |



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 11 1/3/2017 10:32:47 AM

# UTANGULIZI

Takwimu za sensa za mwaka 2012 zinaonesha kwamba wanawake ni 51.7% ya watanzania wote ambao idadi yao ni milioni 44,928,923. Kulingana na takwimu hizi wanawake ni wengi zaidi ya wanaume. Wanawake wengi wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula, kazi za ufundi kama vile ushonaji, udarizi wa nguo, ususi wa nywele, mikeka na biashara ndogondogo ili kuweza kupata mahitaji ya familia. Wanawake pia wanashiriki kwenye kilimo cha mazao ya biashara katika kuongeza nguvu kazi, lakini hawana uwezo wa kumiliki ama kutumia mapato yatokanayo na mazao hayo ambapo mara nyingi huchukuliwa na kumilikiwa na wanaume. Kwa wanawake ambao wanafanya biashara ndogondogo changamoto kubwa imekuwa ni kuwa na mitaji midogo isiyojitosheleza na kukosa dhamana ambayo inaweza kuwasaidia kupata mikopo ili kuongeza mitaji yao.

Japokuwa kitakwimu wanawake ni wengi zaidi ya wanaume, wanawake wanakumbana na changamoto zinazowafanya kushindwa kufurahia matunda ya kazi zao na kuzidi kuongeza umaskini na utegemezi mambo ambayo yanasababisha ukatili wa kijinsia. Utegemezi huo unatokana na mfumo dume hasa kwenye maswala ya mwenye haki ya kumiliki mali au vitu. Mfano halisi ni pale jamii inapowanyang'anya wajane mali pindi wanapofiwa na waume zao, kuwanyima haki ya kumiliki mali kwa mfano ardhi, kufanya kazi na kunyang'anywa vipato na wapenzi au waume zao.

Kutokana na changamoto hizo zinazosababisha ukosefu wa kipato, baadhi ya wanawake na wasichana hujiingiza kwenye biashara zisizo halali ikiwa ni pamoja na biashara ya ngono, na kwa kufanya hivyo wengi wamejikuta wakifanyiwa vitendo vya udhalilishaji hususan



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 12 1/3/2017 10:32:47 AM

kubakwa, kulawitiwa, kupigwa na hata kukashifiwa. Kwa kulitambua jambo hili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kiutekelezaji katika kuandaa sera, mipango, mikakati, sheria na kuridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kikanda yenye lengo la kuondoa ukatili wa Kiuchumi kwa jinsia zote hususan wanawake.

## *Ufafanuzi wa Istilahi*

**Ubaguzi**

Kuwatendea tofauti watu kwa kuzingatia sababu kama vile rangi, dini, jinsi, kabila, umri au vigezo vingine ambavyo vina athari mbaya kwa hisia, au fursa sawa au kutendea katika ajira au kazi. Kuna aina mbalimbali za ubaguzi kama vile 'Ubaguzi wa moja kwa moja', ambao umekuwepo katika taratibu, na 'Ubaguzi wa kisheria' ambao ni ubaguzi katika sheria. Ubaguzi wa Kijinsia unaweza kuwa wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja. Kwa mfano, kuweka vikwazo kwa wanawake au wanaume katika ajira, upandishaji wa vyeo, au mafunzo ni ubaguzi wa moja kwa moja, wakati kuweka vigezo au masharti maalum yanayolenga kuwaondoa ama wanawake au wanaume, ni ubaguzi usio wa moja kwa moja.

**Jinsia**

Tofauti za kijamii baina ya wanawake na wanaume zinazoonekana katika mgawanyo wa kazi, upatikanaji na udhibiti wa vyanzo vya uzalishaji, na uwezo/muundo wa kaya. Mahusiano haya yamejengwa na jamii, ya kujifunza, na yanayobadilika kwa wakati, na yanahusiana na hali ya kiuchumi na muktadha mwingine wa kijamii.

**Ubaguzi wa kijinsia**

Hatua ambazo zinawaathiri wanawake na wanaume kwa mtizamo wa usawa wa kijinsia, Haki, majukumu na fursa sawa kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana kuwa jinsi moja ni dhaifu au ni bora zaidi na si kwa kuzingatia ubora wao halisi.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 13 1/3/2017 10:32:47 AM

**Ukatili Dhidi ya Wanawake**

Ni kitendo au vitendo vya unyanyasaji vyenye kulenga jinsia ya kike na vyenye kusababisha au kuleta madhara ya kimwili, kingono, kihisia, kisaikolojia, kiuchumi na kijamii. Kitendo au vitendo hivi hujumuisha kutumia nguvu na vitisho vya kumnyima mwanamke haki na uhuru.

**Ukatili wa Kiuchumi**

Ni vitendo vya kumnyima mtu fursa ya kupata mahitaji ya msingi na ya kujiendeleza kama kumkataza mke/ mume kufanya kazi, kuzuia fedha za matumizi na kumtolea maneno ya masimango, kejeli wakati wa kumpatia fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kifamilia au binafsi; mfano ununuzi wa mahitaji ya nyumbani, nguo, matibabu, kumnyima mke kushika au kumiliki fedha, kutumia fedha/ mali za familia bila ridhaa ya mwingine mathalan kuendesha gari la familia, kumnyima kumiliki mali na vitendo vingine vinavyosababisha msongo wa mawazo.

**Dhana ya wanawake katika maendeleo**

Ni hatua madhubuti ya kujenga uwezo wa wanawake waweze kujitegemea ili waweze kufanya maamuzi juu ya maisha yao na kutekeleza maamuzi hayo kwa kutumia rasilimali zilizopo bila kuingiliwa au kubughudhiwa na mtu, taasisi au chombo chochote kwa sababu tu, wao ni wanawake.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 14 1/3/2017 10:32:47 AM

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MIKATABA YA KIMATAIFA YA HAKI ZA WANAWAKE KIUCHUMI

### 1.1 MIKATABA YA KIMATAIFA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi nyingi za Afrika zilizoridhia mikataba ya Kimataifa na Kikanda ambayo inaelezea haki za kiuchumi kwa kila mtu. Mikataba hiyo ni pamoja na:-

- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, KIjamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966.
- Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979.
- Mkataba wa Nyongeza wa Afrika wa Haki za Watu na Haki za Binadamu za Wanawake(Itifaki ya Maputo)

Kwa ujumla mikataba hii inatoa wajibu kwa nchi wanachama, Tanzania ikiwemo kuweka fursa na mazingira ya usawa baina ya wanawake na wanaume katika Nyanja ya kiuchumi ili kuwa na maendeleo endelevu.

#### *1.1.1 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966*

Mkataba huu katika ibara ya 2 na 3 unazitaka nchi wanachama kufanya majukumu yafuatayo:- Kuchukua hatua peke yake au kupitia msaada na ushirikiano wa:

- Kuchukua hatua peke yake au kupitia msaada na ushirikiano wa kimataifa hasa hatua za kiuchumi na kiufundi kwa kadri ya hali ya rasilimali zake kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki zilizomo zinafaidiwa hatua kwa hatua kwa njia zote muafaka ikiwemo kupitisha sheria;

- Kuhakikisha watu wake wanafaidi haki bila ubaguzi ( Hapa ina jumuisha watu wote bila kujali jinsi, rangi, au mapungufu ya mtu. Kwa maana nyingine watu wote ikiwemo wanawake walio pembezoni kama vile wenye ulemavu, wazee n.k)
- Kuhakikisha usawa kati ya wanaume na wanawake katika kufaidi haki zilizoorodheshwa kwenye mkataba huu.

Vile vile Mkataba huu unalinda haki za kiuchumi kama vile:-

- haki ya kufanya kazi (ibara ya 6);
- haki ya kufanya kazi katika mazingira mazuri na salama ya kazi ikiwemo kupata chakula, mavazi na malazi (ibara ya 11);
- haki ya kufaidi kiwango cha juu cha afya ya akili na mwili (ibara ya 12);
- haki ya mtu kulindwa kwa familia na ndoa yake (ibara ya 10);
- haki ya hifadhi ya jamii (ibara ya 9).

### *1.1.2 Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW)*

Tanzania ambayo ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) imesaini na imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote Ubaguzi Dhidi ya Wanawake mwaka 1986. Ibara ya 2 ya Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake(CEDAW) inafafanua juu ya wajibu wa nchi wanachama kupambana na kila aina ya ubaguzi dhidi ya wanawake. Wajibu huo ni pamoja na kupitisha sheria zinazofaa, kuweka misingi ya usawa kati ya wanawake na wanaume na kuhakikisha inazingatiwa kupitia Katiba na Sheria za Nchi, Kutunga na kutekeleza sheria zinazofaa au kanuni za udhibiti, na zile zinazozuia na kupunguza aina zote za ubaguzi hasa vitendo vinavyohatarisha ustawi wa wanawake.

Ibara ya 13 inasema nchi mwanachama zinapaswa kuchukua hatua na kutekeleza kisheria pamoja na kuchukua hatua nyingine zitakazowapa wanawake fursa sawa za kuajiriwa na kujiendeleza kitaaluma na fursa


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 16 1/3/2017 10:32:47 AM

nyingine za kiuchumi. Hivyo ili kufikia hayo Serikali itakuwa na Wajibu wa kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuhamasisha usawa katika upatikanaji wa ajira.
- Kuhamasisha haki ya usawa wa malipo kati ya mwanamke na mwanaume kwa ajira yenye thamani sawa.
- Kuhakikisha kuna uwazi kwenye kuajiri, kupandishwa cheo na kufukuzwa kwa wanawake, kutokomeza pamoja na kuadhibu udhalilishwaji wa kingono katika mazingira ya kazi.
- Kuwahakikishia wanawake uhuru wa kuchagua wadhifa wa kazi, na kulindwa kutokana na unyonyaji unaoweza kusababishwa na waajiri wao, wanaokiuka na kuvunja haki zao za msingi kama zinavyotambuliwa na kulindwa na mikataba, sheria na kanuni zenye nguvu kisheria.
- Kuandaa mazingira yanayohamasisha na kutoa kipaumbele kwa nyadhifa na shughuli mbalimbali za kiuchumi za wanawake, hususan katika sekta zisizo rasmi.
- Kuweka mfumo wa utaratibu utakaolinda na kuwapa kinga ya kijamii wanawake wote walio katika sekta zisizo rasmi, ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wafuate mfumo huo.
- Kuweka umri wa chini wa mtu kuajiriwa na kupiga marufuku ajira kwa watoto walio chini ya umri huo. Pia kupiga marufuku pamoja na kutoa adhabu kwa aina zote za unyonyaji kwa watoto, hasa watoto wa jinsi ya kike.
- Kuchukua hatua zinazostahili ili kutambua mchango wa kiuchumi unaotokana na shughuli za kinamama wa nyumbani.
- Kuhakikisha kuna malipo yanayotosheleza kwa wanawake walioajiriwa serikalini na katika sekta binafsi na wanapewa likizo kabla na baada ya kujifungua.
- Kuhakikisha kuna usawa wa matumizi ya sheria za kodi kati ya mwanamke na mwanaume.
- Kutambua na kuzipa nguvu ya kisheria, haki za marupurupu na mapato mengine anayostahilli mwanamke anayelipwa, mshahara sawa sawa na zile wanazopewa wanaume kwa ajili ya wenzi wao na watoto wao.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 17 1/3/2017 10:32:47 AM

Ibara ya 19 inafafanua kuwa wanawake wapate haki ya kufurahia haki zao za kupata maendeleo endelevu kwa nchi wanachama kuhakikisha zinachukua hatua zifuatazo:-

- Kujenga usawa wa kijinsia katka ngazi ya taifa kuhusu mipango ya maendeleo.
- Kuhakikisha ushiriki wa Wanawake katika ngazi zote za kutoa maamuzi na utekelezaji wa maendeleo ya sera na program.
- Kusimamia Wanawake kupata ardhi na kupata hati za umiliki.
- Kuhamasisha upatikanaji wa mikopo kwa wanawake, mafunzo, ujuzi endelevu na kupanua huduma hizo mijini na vijijini katika ngazi zote ili kuwapatia wanawake maisha bora na kupunguza kiwango cha umasikini kwa wanawake.
- Kutilia maanani viashiria vya maendeleo ya binadamu hasa kwa wanawake, kuhusiana na maendeleo ya sera ya mipango.
- Kuhakikisha kuwa madhara ya utandawazi na madhara ya mipango ya kibiashara na sera hayamuathiri mwanamke.

**Wajibu wa Serikali katika kuinua Haki za Kiuchumi**

- Serikali inawajibika kuhakikisha kwamba watu wote wanawake kwa wanaume bila kujali rangi, jinsi, lugha, dini, siasa, kabila, hali ya mtu au mahali alikotoka, wanapata fursa sawa za kiuchumi na wanatumia fursa hizo bila ubaguzi wa namna yoyote ile.
- Serikali haipaswi kutengeneza sheria itakayowanyima watu fursa ya kutengeneza umoja wao wa Kiuchumi na kibiashara.
- Serikali inawajibika kuhakikisha kwamba watu wananufaika na kutumia ipasavyo rasilimali za nchi na utajiri wake.
- Bila kuathiri haki za watu wengine serikali inatakiwa kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake.
- Serikali inawajibika kuhakikisha kwamba utajiri wa taifa unaendelezwa, unahaifadhiwa na unatumiwa kwa manufaaa ya wananchi wote kwa ujumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 18 1/3/2017 10:32:48 AM

- Serikali na vyombo vyake vyote vya umma vinawajibika kutoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu. Pia serikali inawajibika kuhakikisha kwamba aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu na upendeleo vinaondolewa nchini.
- Serikali itahakikisha kwamba matumizi ya utajiri wa taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa yanaelekezwa kwenye jitihada ya kutokomeza umaskini, ujinga na maradhi.
- Serikali itahakikisha kwamba shughuli za Kiuchumi haziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za Kiuchumi katika mamlaka ya watu binafsi walio wachache.


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 19 1/3/2017 10:32:48 AM

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 SERA, MIPANGO NA SHERIA ZA TAIFA ZINAZOLINDA NA KUINUA UCHUMI WA WANAWAKE

### 2.1 SERA ZA KITAIFA ZINAZOLENGA KUINUA UCHUMI WA WANAWAKE

Katika kutilia mkazo na kama sehemu ya kuridhia mikataba ya Kimataifa iliyotajwa hapo juu na katika kutekeleza wajibu wake; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonyesha nia yake ya wazi kwa kupinga ukatili wa Kiuchumi kwa kuandaa sera, mipango na Sheria mbalimbali ili kutoa fursa sawa ya Kiuchumi hususan kwa wanawake. Baadhi ya Sera na Mipango hiyo ni pamoja na:-

- **Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000**; Sera hii imelenga kushughulikia upungufu na kukosekana kwa usawa kati ya wanaume na wanawake kwa kuhusianisha suala la rasilimali, umaskini na kuupa thamani mchango wa wanawake katika maendeleo ya Taifa.
- **Sera ya Ajira ya mwaka 2008**, serikali inahimiza ajira zenye staha, uzalishaji na imedhamiria kuweka usawa katika nafasi zilizopo na kuhakikisha rasilimali zilizopo zinayafikia makundi yaliyopo pembezoni wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hii inamaanisha kuelekeza zaidi uwekezaji wa rasilimali kwa sekta kama vile kilimo, shughuli zisizo za kilimo vijijini, uzalishaji na usindikaji wa mazao zinazoweza kuzalisha ajira kwa wingi. Inategemewa kwamba kuelekeza rasilimali katika sekta tajwa hapo juu kutawezesha upatikanaji wa ajira hasa kwa wanawake na vijana walioko mijini na vijijini na hata pembezoni.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 20 1/3/2017 10:32:48 AM

## 2.2 MIPANGO YA TAIFA

**I. Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2016/2017-2021/2022).**

Mpango huu una lengo la kutokomeza ubaguzi na unyonyaji wa kisheria, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa unaoathiri wanawake na watoto. Mpango huu pia unalenga kuongeza juhudi za Serikali kwa kushirikiana na wadau kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuhakikisha usawa na haki kati ya wanawake na wanaume nchini Tanzania.

**II. Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA II)**

Mpango huu umeainisha njia za kuendeleza na kulinda haki za binadamu kwa watu wote hasa kwa wanawake na wanaume maskini, watoto, watu wanaoishi katika hali hatarishi na makundi maalumu (angalia MKUKUTA II-kundi la III, lengo la 3) na kuongeza uzalishaji na fursa za ajira zenye tija na stahifu hususan kwa wanawake na vijana (angalia MKUKUTA II kundi la I, lengo la 3) ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Mpango huu pia umelenga kuhakikisha watekelezaji wa sheria wanaelimishwa juu ya haki za wanawake hususan haki ya kumiliki mali, pia kuhakikisha kwamba wanawake wanapata mikopo kutoka taasisi za mikopo ili kujikwamua kiuchumi kutoka kwenye lindi la umaskini. Aidha, kutoa elimu kwa umma juu ya haki za wanawake na jinsi mila na desturi zinavyosababisha wanawake kutokushiriki kikamilifu katika masuala ya uchumi.

Changamoto iliyopo ni ukosefu wa kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa ahadi hizi kwa wanawake na vijana kwa kuelekeza rasilimali za kutosha na kutekeleza mikakati katika kuleta hali ya kijamii na kiuchumi kwa wanawake na vijana, hivyo kupunguza hali hatarishi ya Ukatili wa kijinsia.


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 21 1/3/2017 10:32:48 AM

MKUKUTA, pia umelenga kuhamasisha skimu zinazoweza kuwapatia kipato wasichana waliofikia katika umri wa kuvunja ungo na wanawake ikijumuisha upatikanaji wa mikopo kama mojawapo ya mkakati wa kinga ya jamii.

III. **Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa Mwaka (2013-2017)** Mpango huu unatekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika mambo unayoyazingatia ni pamoja na kuhakikisha kwamba kunakuwepo na haki sawa, mipango na sera zinazomwezesha mwanamke kushiriki kikamilifu katika masuala ya kiuchumi , kisiasa na kijamii.

## 2.3. SHERIA NA HAKI ZINAZOLINDA NA KUINUA UCHUMI WA WANAWAKE

Serikali inatambua uwepo wa tatizo la ukatili wa kijinsia Kiuchumi husuan kwa wanawake. Hivyo basi, serikali imetunga sheria mbalimbali kuweza kuhakikisha uwepo wa fursa na haki sawa za Kiuchumi baina ya wanawake na wanaume kwa ajili ya maendeleo endelevu. Sheria hizo ni pamoja na:

### *2.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977*

Katiba ni sheria mama ya nchi. Ibara ya 12 na 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kwamba watu wote ni sawa na wanahaki sawa bila ya ubaguzi wowote.Katiba inakataza ubaguzi wa aina yoyote ile na kumbagua mtu kwa misingi ya ukabila, utaifa, pahala mtu alipotokea, maoni ya kisiasa, dini, jinsi au hali yao ya maisha kwa namna ambayo watu wa aina fulani wanafanywa na kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 ibara ya 22-23 inaeleza kwamba kila mtu anayo haki ya kufanya kazi, kupata ujira


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 22 1/3/2017 10:32:48 AM

wa haki na kushika nafasi yeyote ya kazi iliyo chini ya mamlaka kwa usawa bila ubaguzi wa aina yoyote kulingana na uwezo na sifa ya kazi anayofanya. Nia ya serikali ni kuhakikisha uwepo wa fursa sawa katika ajira zinazofikiwa ama kupatikana kwa wanaume na wanawake.

**Haki ya kumiliki mali na fidia bila ubaguzi**

Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inakataza mtu kunyang'anywa mali yake, au kutaifishiwa mali yake bila kupewa fidia.

Ili kusisisitiza jambo hili, Sera ya Taifa ya Ardhi ya 1995 imetamka bayana kwamba pale ambapo ardhi inatwaliwa basi fidia ya haki na iliyo kamili itolewe kwa mtu ambaye haki yake ya umiliki inafutwa au inaingiliwa na maslahi yake yanaathiriwa kwa ajili ya manufaa ya umma.

### *2.3.2 Sheria za Ardhi za Mwaka 1999*

Katika kuhakikisha kwamba uwepo au upatikanaji wa fursa na haki sawa ya umiliki wa mali. Sheria za Ardhi Na.4 na 5 za mwaka 1999 zilitungwa ili kuondoa ubaguzi wa kijinsia kwenye masuala yahusuyo ardhi na kutoa fursa sawa kwa wanawake katika umiliki wa rasilimali ya ardhi.

Kwa mfano; kifungu cha (3) cha Sheria za Ardhi Na.4 na 5 za mwaka 1999 kinatoa fursa na haki sawa katika upatikanaji, umiliki, utumiaji, uuzaji, ugawaji na ukodishaji wa ardhi kwa masharti na viwango sawa baina ya wanawake na wanaume.

Kuna baadhi ya makabila ya Tanzania ambayo hayakubali wanawake kumiliki ardhi au mashamba ya ukoo. Hii inatokana na mila na desturi za sehemu husika, ambazo zinawanyima wanawake fursa ya kumiliki mali. Hata hivyo, kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Ardhi ya Kijiji, kinabatilisha sheria zote za mila zinazowabagua wanawake. Kifungu hicho kinaeleza kwamba; "kanuni au sheria ya kimila na uamuzi wowote unaochukuliwa kama ni kuhusu ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi au jumuiya, itazingatia



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 23 1/3/2017 10:32:48 AM

mila, desturi na mazoea ya jamii inayohusika kwa kiasi ambacho kinawiana na misingi na Sera ya Taifa ya Ardhi ama sheria nyingine yoyote na bila kuathiri masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki, kanuni hiyo ya sheria ya kimila au uamuzi huo kuhusu ardhi inayomilikiwa kwa miliki ya kimila vitakuwa batili na havitatumika wala kutekelezwa na Halmashauri yoyote ya kijiji au Mkutano Mkuu wa Kijiji chochote au mtu yeyote au kundi lolote la watu wanaotekeleza mamlaka yoyote kuhusu ardhi ya kijiji au kuhusu mahakama yoyote au chombo kingine chochote, kwa kiasi ambacho inawanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu njia halali za kumiliki au kutumia ardhi yoyote kama hiyo.

Kwa hiyo basi, Sheria hii inakataza mila na desturi ambazo zinawabagua wanawake, watoto na watu wenye ulemavu. Hivyo, ni Wajibu wa kila mwanajamii na vyombo vya utekelezaji wa maamuzi vya serikali kuhakikisha kwamba hakuna ubaguzi wa kijinsia katika masuala ya haki ya uchumi hususan kwenye suala la ardhi.

Aidha kwa wanandoa ambao wanataka kuuza au kuweka rehani ardhi au mali iliyopatikana wakati wa ndoa ni wajibu wa mwanandoa kupata idhini ya mwanandoa mwenzie. Jambo hili limesisitizwa pia kwenye shauri la daawa la ***Mtumwa Rashid dhidi ya Abdalla Iddi, Rufaa Na.22/1993(Masjala ya Dares Salaam)*** ambapo Mahakama ya Rufani ya Tanzania iliamua kwamba mkataba wa mauziano ya nyumba ni batili kwa kukosa idhini ya mwanandoa mwenzie, hata kama mali hiyo imesajiliwa kwa jina la mmoja wa wanandoa chini ya Kifungu Na.60 cha Sheria ya Ndoa ya 1971.

Maamuzi haya ya mahakama yalitolewa kwa kuzingatia usawa na haki katika upatikanaji wa mali za wanandoa hasa mali kama vile nyumba na ardhi. Hivyo basi ni vyema mtu yeyote anapotaka kununua au kuweka rehani mali iliyopatikana wakati wa ndoa, ahakikishe anapata idhini ya mwanandoa mwingine, vinginevyo yule ambaye atawekeshewa rehani au atanunua mali hiyo ategemee hasara kwa kuwa makubaliano hayo yatakuwa batili iwapo mwanandoa mmoja ataonekana hakutoa ridhaa/idhini.


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 24 1/3/2017 10:32:48 AM

Kwa mfano Sheria ya Ardhi ya Kijiji Kifungu cha 22(3) kinaeleza na kutoa haki kwa mwanamke ambaye ni raia wa Tanzania, hata kama ametalikiwa au alimwacha mume wake kwa kipindi kisichopungua miaka miwili aweze kupatiwa ardhi ya kijiji iwapo atawasilisha maombi yake. Serikali imeweka kifungu hiki ili kulinda maslahi ya wanawake ambao wametalikiwa.

Katika kuhakikisha kuwa haki ya kumiliki mali hususan ardhi inalindwa kwa mwanamke Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na.5/1999 inatoa Wajibu kwa Kamati ya Uamuzi ya Kijiji kulinda maslahi ya wanawake na watoto wasiokuwepo kijijini pale ambapo ardhi zao zinataka kuvamiwa au kutwaliwa na mtu au taasisi yoyote.

### *2.3.3 Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971*

Kwa mujibu wa vifungu vya 56 na 58 vya Sheria ya Ndoa, mwanamke aliyeolewa ana haki sawa ya kupata, kumiliki na kutumia mali yake kama ilivyo kwa mwanaume. Ifahamike kuwa mwanamke aliyeolewa kwa mujibu wa Sheria hii ana haki ya kumiliki mali yake aliyoipata kabla ya ndoa na hata baada ya ndoa. Ana haki ya kuuza mali yake mwenyewe isiyohamishika na inayohamishika kama ilivyo kwa mwanaume. Mali isiyohamishika ni pamoja na nyumba, mashamba. Mfano wa mali inayohamishika ni pamoja na mazao, gari.

Mke / mume ana haki ya kupata mgawanyo sawa wa mali zilizochumwa wakati wa ndoa hata kama hakutoa pesa ya moja kwa moja katika upatikanaji wa mali hiyo. Kwa mfano kazi za nyumbani anazozifanya mwanamke ni mchango tosha katika upatikanaji wa mali za wanandoa. Kulima au kusimamia ujenzi wa nyumba ni mchango tosha katika upatikanaji wa mali za wanandoa. Msimamo huu wa kupata mgawanywo wa mali za ndoa, pale ndoa inapovunjika ulitolewa na mahakama katika kesi ya ***Bi Hawa Mohamed dhidi ya Ally Sefy(1983***) kwamba hata kama mume alichangia kwa hali na mali, mchango wa


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 25 1/3/2017 10:32:48 AM

mama wa nyumbani katika majukumu ya nyumbani unamfanya astahili kupata sehemu ya mali iliyochumwa.

### 2.3.4 Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004

Sheria hii inaharamisha ubaguzi wa aina yoyote kwenye masuala ya ajira na mahali pa kazi, ikiwemo ubaguzi wa moja kwa moja na ule usio wa moja kwa moja kwa mfano, ubaguzi wa rangi, kabila, dini, kisiasa, jinsi, jinsia, ubaguzi kutokana na ujauzito, hali ya ulemavu, umri na ubaguzi kutokana na hali ya kimaisha aliyonayo mtu.

### 2.3.5 Sheria ya Leseni za Biashara Na. 208 /2002

Serikali inatambua kwamba kuna wananchi wengi ambao wamejiajiri kwenye sekta binafsi na wanaendesha biashara mbalimbali ili kuweza kujipatia kipato. Ni kwa mantiki hiyo serikali imeweka sharti kwa mfanyabiashara kuwa na leseni ili aweze kuendesha biashara yake kihalali. Mfanyabiashara aliye na leseni anapaswa kuendesha biashara yake kulingana na aina ya leseni aliyoomba. Mfano, kama mwombaji ameomba leseni yake kwa ajili ya biashara ya kuuza vipodozi anatakiwa auze vipodozi na siyo vinywaji baridi.

Kwa kawaida, leseni hutolewa na mamlaka mbalimbali za serikali kama vile EWURA, TFDA, CRB. Mamlaka nyingine za serikali zinazotoa leseni ni pamoja na ya serikali za Mitaa ambazo zinaweza kutunga sheria ndogo zitakazowapa mamlaka ya kutoza ada ya leseni za biashara kwa aina tofauti tofauti kwa kushaurina na Waziri wa Viwanda na Biashara mwenye dhamana na kwa kupitishwa kwa Waziri wa Fedha mwenye dhamana.

Halmashauri za vijiji pia zinaweza kutunga sheria ndogo zitazowawezesha kutoza ada ya leseni za biashara kwenye eneo lao.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 26 1/3/2017 10:32:48 AM

**Kumbuka:** Kuwa na leseni husaidia mfanyabiashara kuweza kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha hivyo kuongeza mtaji wake na hatimaye kujikwamua kiuchumi.

### *2.3.6 Sheria ya Majina ya Biashara Na. 231*

Biashara binafsi na zenye ubia ni moja ya mifano ya biashara zinazosajiliwa chini ya sheria hii. Jina la biashara linasaidia kutambulisha biashara yako na hivo kuitangaza biashara yako kwa wateja wako.

(I) **Usajili wa Biashara ya mtu binafsi**

Watu wengi hupenda kusajili biashara zao kwa stahili hii kwa kuwa ni rahisi katika uanzishaji na usimamizi. Biashara ya mtu binafsi humilikiwa na mtu mmoja kwa jina lake, hivyo basi atakuwa na wajibu wa kuratibu shughuli zote za biashara, kulipa kodi anayotakiwa na madeni na leseni ya biashara kutoka halmashauri au manispaa anayofanyia biashara yake.

Mfano wa jina la biashara binafsi unaweza ukawa ***'MZURI KWAO BOTIQUE'***

(II) **Biashara zenye ubia**

Mahusiano ya biashara hii yanatokana na mkataba ambapo watu kuanzia wawili wataingia mkataba wa ubia kwamba wanania ya kufanya biashara kwa pamoja na kupata faida.

**Kumbuka:** Tofauti kati ya usajili wa biashara ya mtu binafsi na biashara zenye ubia ni kwamba usajili wa ubia unahusu watu wawili au zaidi lakini wasiozidi ishirini wenye lengo la kufanya biashara ili kupata faida.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 27 1/3/2017 10:32:48 AM

(III) **Sheria za Makampuni (haki ya usajili wa biashara kama kampuni)**

Zifuatazo ni sheria zinazowezesha mtu kuweza kusajili biashara yake kama kampuni ya biashara ya mtu au watu binafsi. Sheria hizo ni pamoja na:

(a) Sheria ya Makampuni Na. 212/ya Mwaka 2002

(b) Sheria ya Mikataba sura 345 kama ilivyorejewa Mwaka 2002

(c) Kanuni za Kufungua Kampuni ya Mwaka 1929

(d) Kanuni za Makampuni ya Mwaka 2003

**Faida za kuwa na kampuni ni pamoja na: -**

(i) Kutambulika kisheria

(ii) Kumiliki mali kwa jina la kampuni

(iii) Kuweza kumiliki hisa (mali).

(iv) Kufaidika na punguzo la viwango vya kodi.

**TARATIBU ZA KUFUATA ILI KUSAJILI JINA LA BIASHARA**

(a) Mwombaji atapaswa kujaza fomu ya kuombea jina la biashara

- Iwapo mwombaji ni mtu binafsi atajaza fomu Na. 3 kama inavyoonekana kwenye *Kiambatanisho 1*.
- Waombaji wakiwa kwenye ushirika/kikundi watapaswa kujaza fomu Na. 8
- Mwombaji/waombaji watapaswa kufanya uchunguzi kama jina lilishatolewa au la Mwombaji anaweza kutafuta jina lake kwenye tovuti ya Msajili wa Makampuni na baada ya siku tatu atajulishwa jina analoomba kutumia kwenye biashara yake kama linatumika au la. Au anaweza kufika kwenye ofisi za Msajili wa Makampuni (BRELA) kwa usaidizi zaidi.
- Msajili wa makampuni (BRELA) anaweza kukubali au kukataa jina husika iwapo jina hilo la biashara linatumika na mtu/watu wengine.
- Jina likikubaliwa mwombaji atapaswa kulipia ada na atapewa cheti cha usajii wa biashara yake. Msajili atakituma cheti hiki kwenye barua pepe ya mwombaji na kwenye sanduku la barua au kumpa mhusika ana kwa ana.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 28 1/3/2017 10:32:49 AM

## LESENI YA BIASHARA

### Masharti ya Kupata Leseni ya biashara

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ili mradi:

- Awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane na kuendelea
- Awe na akili timamu, ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai (katika kipindi cha miezi kumi na mbili iliyopita) kabla hajaoamba leseni ya biashara.
- Awe na eneo la kufanyia biashara linalotambulika kisheria.

### Utaratibu wa Kupata Leseni ya Biashara

Mwombaji anapaswa kujaza fomu ya maombi TFN 211 kikamilifu na kuambatanisha kivuli cha:

- Nakala ya hati ya usajili (*certificate of incorporation*) iwapo ni kampuni na *certificate of registration and extract* kama amesajili biashara yake kwa jina la biashara binafsi.
- Kama biashara yake ni ya kampuni basi aambatanishe na katiba ambayo inaonesha kipengele ambacho kampuni inaombea leseni ya biashara.
- Hati ya kusafiria ya Tanzania au kiambatanisho cha uraia au kitambulisho cha mpiga kura au hati ya kiapo kuonyesha kuwa yeye ni mtanzania.
- Hati ya kiuwakili (power of attorney), iwapo wenye hisa wote wa kampuni wapo nje ya nchi, itolewe kwa mtanzania ambaye anaishi hapa nchi.
- Ushahidi wa maandishi kuwa ana mahali pa kufanyia biashara mfano: mkataba wa pango, risiti za malipo ya kodi za majengo au ardhi au hati ya nyumba ambapo biashara ipo.
- Hati ya kujiandikisha kama mlipa kodi inayotolewa na Mamlaka ya Kodi Tanzania ijulikanayo kama (TIN)
- Kwa leseni zinazodhibitiwa na mamlaka mbalimbali (EWURA, TFDA, TALA) ,kwa biashara za utalii au mahoteli ya kitalii) mwombaji hana budi kuwa na leseni husika kabla ya kuomba leseni ya biashara.
- Hati/cheti cha utaalamu kwa biashara zote za ushauri wa kitaalamu kwa mfano: leseni za kuendesha hospital, zahanati, udaktari, uhandisi, urubani wa ndege, nahodha wa meli, hati


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 29 1/3/2017 10:32:49 AM

zinazohusu chombo kufanya kazi ya uchukuzi (air worthiness kwa ndege na sea worthiness kwa meli) uwakili.

Mwombaji akikamilisha viambatanisho hivi vyote, ni vyema aviwasilishe kwenye ofisi za halmashauri ya wilaya au mji ili aweze kupatiwa leseni ya biashara.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 30 1/3/2017 10:32:49 AM

# SEHEMU YA TATU

## 3.0. SHERIA ZINAZOATHIRI FURSA ZA WANAWAKE KIUCHUMI

### 3.1 SHERIA YA KIMILA YA MWAKA 1963 - TANGAZO LA SERIKALI NA.436 /LA MWAKA 1963

Sheria hii inatumiwa na watanzania wote wazawa wanaofuata mila na desturi zao na wanaorithi kupitia upande wa baba. Sheria ya kimila ni ya kibaguzi na huleta changamoto kwa wanawake, wajane na watoto ambao wamezaliwa nje ya ndoa, hususan katika urithi wa mali.

Kushindwa kurithi mali mfano ardhi kunawakosesha wajane kipato. Hali hii imesababisha baadhi kukubaliwa kurithiwa na ndugu wa marehemu au kufanyiwa utakaso ili waweze kuendelea kutumia mali walizochuma na wenzi wao. Vitendo hivi ni ukatili wa kijinsia na vinachangia kuenea kwa UKIMWI na maambukizi mapya.

Kwa mujibu wa sheria hii mgawanyo wa mali ya marehemu upo katika madaraja matatu:

i. **Daraja la kwanza (1) -** Mtoto wa kwanza wa kiume ambaye anapata fungu kubwa kuliko watoto wengine wote wa marehemu
ii. **Daraja la pili (2)** - Watoto wengine wa kiume waliobaki, hawa wanapata fungu kubwa kiasi na
iii. **Daraja la tatu (3) -** Watoto wa kike bila kujali umri na hali katika familia. Watoto wa kike wa marehemu hurithi fungu dogo na hunyimwa haki ya kumiliki ardhi.
iv. **Mjane: -** Kwa mujibu wa sheria hii, mjane hana haki ya kurithi mali yoyote kutoka kwa marehemu mume wake isipokuwa huchukuliwa kuwa atatunzwa na watoto wake. Mjane ambaye hajabahatika kuzaa, hupata asilimia 20 ya asilimia 50 ya mali za marehemu mume wake.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 31 1/3/2017 10:32:49 AM

## 3.2. SHERIA YA NDOA YA 1971

Kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 114 wakati wa kuvunja ndoa , mahakama inatakiwa kugawa mali zilizochumwa kwa pamoja na wanandoa wakati wa ndoa yao. Kabla ya kutoa maamuzi ni kiasi au aina gani ya mali anapaswa mwanandoa kupewa, ***mahakama inapaswa kuangalia pamoja na mambo mengine kiwango cha mchango wa kila mwanandoa katika kuchuma mali***. Uzoefu umeonyesha kwamba wanawake wanabeba mzigo mkubwa mfano wa kutunza wagonjwa, kulisha familia. Shughuli hizi kwa bahati mbaya hazithaminishwi kifedha na mahakama kama moja ya mchango katika upatikanaji wa mali za wanandoa, kwani muda mwingi umetumika wakati wanayatekeleza majukumu haya. Kwa hiyo ndoa inapovunjika mwanandoa hususan mwanamke anapewa fungu dogo la mali kuliko mwenzi wake kwa kuwa hana risiti anayoweza kuionyesha mahakamani kama ushahidi wa gharama ya muda na nguvu aliotumia kutunza familia au mgonjwa wakati mume akiendelea na utafutaji wa kipato ambao anaweza kupeleka mahakamani(mfano hati za malipo ya mshahara), au leseni ya biashara na mahakama ikampa haki. Jambo hili ni la ukatili kwa kuwa mchango wa mwanaume unaonekana kuwa mkubwa kuliko mwanandoa mwanamke katika upatikanaji wa mali za ndoa.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 32 1/3/2017 10:32:49 AM

# SURA YA NNE

## 4.0. TAASISI ZA KIFEDHA NA MFUKO WA WANAWAKE KATIKA KUKUZA UCHUMI

### 4.1. BENKI YA WANAWAKE YA TANZANIA (TWB)

Katika kuhakikisha kuwa Wanawake wanachangia pato la Taifa kupitia shughuli mbalimbali za uzalishaji mali serikali imeanzisha benki ya Maendeleo ya Wanawake (TWB) ambayo inalenga kuwainua wanawake Kiuchumi hasa wanawake wenye kipato cha chini, kati na wajasiriamali wadogo ambao wanashindwa kukopa kwenye taasisi za kifedha zingine kwa sababu ya riba kuwa za juu, kutokuwa na dhamana na pia wanawake wa vijijini. Nia ya benki hii ni kupeleka huduma zake kwenye mikoa yote ya Tanzania. Hata hivyo mpaka sasa benki hii ina matawi manne yaliyoko katika mikoa ya Dares Salaam (matawi mawili) Mwanza na Dodoma.

### 4.2. HUDUMA ZA BENKI NYINGINE

Mbali na benki ya wanawake, benki nyingine hapa nchini pia hutoa huduma za kifedha katika kuhakikisha wanawake wanapata mikopo kwa riba nafuu kulingana na kiasi cha fedha anazokopa. Benki hizo ni pamoja na;

1. Benki ya NBC
2. Benk ya CRDB
3. Benki ya Mkombozi
4. Benki ya Amana
5. Vision Fund Tanzania
6. Twiga Bancorp
7. Benki ya Maendeleo



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 33 1/3/2017 10:32:49 AM

8. Benki ya jumuiya ya Mufindi
9. Benki ya Posta
10. Benki ya jumuiya ya Meru
11. FINCA
12. Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB)
13. Benki ya Biashara ya Kenya (KCB)

**Angalizo:** Benki zote tajwa hapo juu zinatoa mikopo kwa mtu binafsi au vikundi vya watu kulingana na mahitaji. Hivyo basi ni vyema mtu akachambua kwa undani na kutathmini ni benki ipi yenye riba na masharti nafuu kabla ya kuchukua mkopo anaoutaka.

## 4.3. MFUKO WA WANAWAKE KATIKA KUKUZA UCHUMI (WDF)

Lengo kuu la mfuko huu ni kutoa mikopo kwa wanawake kwa ajili ya kuinua uchumi wa wanawake katika kila Halimashauri. Wizara ya Maendeleo, Jinsia na Watoto huchangia pesa kwenye mfuko huu na halmashauri nazo hupaswa kuchangia pesa kwenye mfuko huu ili kuwawezesha wanawake kupata mikopo ili kuondokana na utegemezi kwa wanaume na kuinua vipato vyao na kuondokana na umaskini.

## 4.4. BENKI ZA KIJAMII NA TAASISI NDOGO NDOGO ZA FEDHA

### *4.4.1 Benki za Kijamii Vijijini na Mjini (VICOBA)*

Neno VICOBA ni kifupi cha maneno ya kiingereza yanayomaanisha ‘Village Community Bank’ likiwa na maana ya Benki ya Kijamii Vijijini. Mfumo wa VICOBA ni mfumo ambao umemlenga mtu wa hali ya chini, kumpatia mtaji na kumwezesha kujiunga katika shughuli za kiuchumi za kuongeza kipato. VICOBA ni tofauti na benki nyingine ambazo huelekezwa kwenye gharama za uendeshaji kama vile mishahara ya wafanyakazi na matumizi mengine hivyo kusababisha kutokidhi lengo la kuondoa umaskini na faida ndogo kwa wanahisa au wateja wake,



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 34 1/3/2017 10:32:49 AM

- Mfumo unalenga zaidi kumjengea uwezo mwanachama kwa kumpa elimu kabla ya kuanza kufanya shughuli za kiuchumi na biashara. Pia unamuwezesha mwanachama kupata mtaji wa kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi za uzalishaji mali na biashara.
- Kikundi kimoja cha VICOBA huundwa na wanachama wapatao 30 ambao hupatiwa mafunzo, huweka hisa, huchukua mikopo na kuendesha shughuli za kiuchumi za uzalishaji mali na biashara.

### 4.4.2. Sifa za mfumo wa VICOBA

- VICOBA ni mradi unaomilikiwa kwa ujumla na jumuiya zilizolengwa
- VICOBA ni mfumo ambao jamii ambayo maisha yake ni ya kiwango cha chini ya mstari wa umasikini inamudu kuutumia.
  i. VICOBA inaweza kutumiwa kama njia mbadala kupitishia elimu katika shughuli za kijamii.
  ii. VICOBA inafuata mfumo wa kimaamuzi kutoka chini kwenda juu katika maeneo ya upangaji, utekelezaji na umiliki.

### 4.4.3. Faida za kuunda na kujiunga na VICOBA

1. Kupata fursa ya mafunzo ya **KUJITAMBUA, FEDHA, UJASIRIAMALI** na **UWEKEZAJI** na kukuwezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi na uzalishaji mali kwa mtizamo chanya, uelewa na ujuzi mkubwa.
2. Kupata fursa ya kukutana na watu mbalimbali toka serikalini, sekta binafsi, wabia wa VICOBA nk katika mafunzo, mikutano, semina, makongamano, uzinduzi na sherehe mbalimbali na kubadilishana ujuzi, mbinu na uzoefu katika shughuli za kifedha, kiuchumi, kijamii na mfumo mzima wa maisha ya kila siku na maendeleo endelevu ndani na nje ya nchi.

3. Kupata fursa za huduma za fedha kama vile;
   - Kuwa na akiba yako
   - Kuwa na mfuko wako wa jamii


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 35 1/3/2017 10:32:49 AM

- Kupata mkopo kwa urahisi
- Kuwa na bima
- Kupata mfumo wa malipo kwa urahisi (kielektroniki nk).

Huduma hizi za kifedha kwa sasa zimeanza kutolewa na benki ya Posta ambayo ina matawi Tanzania nzima. Ni wito wa shirika la WiLDAF kwa wanawake kutumia fursa hii kufungua akaunti za VICOBA kwenye benki hii ili kuweza kunufaika na fursa zilizopo.

4. Kupata fursa ya kuwa mwalimu wa VICOBA na kuwafundisha wengine mfumo wa VICOBA endelevu, kujitambua na kujitegemea, ujasiriamali na fedha.

### *4.4.4. Vikwazo katika uundwaji na uendeshaji wa VICOBA*

- Mila na Desturi katika jamii. Jamii hususan wanaume kuamini kwamba wanawake wakijiunga kwenye VICOBA watatajirika na kutowaheshimu, kwa hiyo sehemu nyingine vikundi vimeshindwa kuanzishwa.
- Uelewa mdogo kuhusu uendeshaji wa VICOBA (mijini na vijijini)
- Ukosefu wa fedha katika kuanzisha na kuendesha VICOBA. Mara nyingi viwango vya mikopo vinavyotolewa wakati kikundi kinaanzishwa huwa vidogo na kiwango hutolewa kulingana na hisa ambazo mwanakikundi anazo.
- Mikopo kutopatikana kwa wakati unaopaswa kama wanakikundi wasiporejesha mikopo kwa wakati uliopangwa.
- Kutokuwepo kwa sheria, sera ya jinsi ya kuendesha VICOBA kama ilivyo kwa taasisi nyingine za kibenki.

### *4.4.5. Mfumo wa Usajili wa VICOBA*

- Mpaka sasa hakuna utaratibu maalumu uliowekwa hivyo usajili wa VICOBA hutegemea maamuzi ya wanakikundi. Hata hivyo


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 36 1/3/2017 10:32:49 AM

wanakikundi katika VICOBA wanaweza kusajili VICOBA chini ya sheria zifuatazo:-

- Sheria ya Makampuni Sura ya 212 ya 2002 ambayo lengo lake kuu litakuwa kuendesha shughuli za VICOBA.
- Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20/2003 na kanuni za ushirika za mwaka 2004. Kwa mujibu wa sheria hii watu ishirini au zaidi wanaweza kuunda ushirika wa kuweka na kukopa. Pia ushirika unaweza kuwa na biashara za rejareja na jumla miongoni mwa wanachama.
- Sheria ya Kusajili mashirika yasiyo ya Kiserikali ya 2002, ambapo wanakikundi itabidi waandae katiba na moja ya malengo yake ni kufanya shughuli za kuweka na kukopa. Masharti mengine ya kufanya usajili ni pamoja na kuambatanisha picha ndogo, nakala za wasifu (CV) za viongozi wa kikundi, barua toka Halmashauri VICOBA ilipoanzishwa, muhutasari ulioridhia uanzishwaji wa kikundi. Muhustari huu unapaswa kusainiwa na wanakikundi wote. Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali anapatikana katika Ofisi za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto zilizopo Dares Salaam.
- Sheria ya usajili wa majina ya Biashara Sura 213 ya 2002. Wanakikundi wanapaswa kupendekaza jina la biashara na baada ya kusajili watapaswa kuendesha biashara yao kufuatana na katiba yao.

## 4.5. SACCOS

### *4.5.1. Kuhusu SACCOS*

SACCOS ni Asasi ya fedha ya ushirika inayoundwa na watu waliojiunga pamoja kwa hiari yao wenyewe ambao wamekubaliana kuweka fedha zao pamoja na kukopeshana kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi na kijamii. Wanachama wa SACCOS mara nyingi huwa na lengo au kitu kinachowaweka pamoja. Lengo au kitu hicho kinaweza kuwa eneo wanaloishi, ajira, imani za kidini (kusali katika msikiti, kanisa na au dhehebu au dini moja) n.k.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 37 1/3/2017 10:32:49 AM

Mfumo wa SACCOS unatambulika kisheria na umeainishwa katika sera ya fedha na uendeshaji wa taasisi za kifedha na unasajilliwa chini ya msajili wa vyama vya ushirika. Sheria inayotumika sasa ni ya mwaka 2003. Mfumo wa SACCOS kwa mara ya kwanza uliingizwa hapa Tanzania mwaka 1954.

SACCOS huongozwa na Bodi ambayo inakuwa na wajumbe wasiozidi tisa. Bodi huajiri watendaji wenye taaluma ya SACCOS au uendeshaji wa mifumo ya kifedha. Kwa mujibu wa sheria, SACCOS huanzishwa na wanachama kuanzia ishirini na hakuna kikomo cha juu cha idadi ya wanachama. Vile vile; SACCOS ni lazima iwe na ofisi na wafanya kazi. Kwa kawaida ofisi inatakiwa iwe na chumba maalum ambacho kinaitwa strong Room kwa ajili ya kutunzia fedha na nyaraka za SACCOS.

### *4.5.2. Taratibu rasmi za kuanzisha SACCOS*

1. Kuhakikisha idadi ya wanachama haipungui watu watano. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) cha sheria ya Vyama vya Ushirika. Hata hivyo idadi hii ni kwa waanzishaji wa awali. Hii ni kwa kuwa idadi hasa inayotakiwa ni kuanzia watu ishirini. Msajili wa vyama vya ushirika hutoa maelekezo ya idadi kwa namna anavyoona inafaa kulingana na kikundi husika.
2. Kwenda kwa msajili wa vyama vya ushirika ambaye hupatikana katika kila makao makuu ya wilaya husika. Nenda makao makuu ya wilaya na uliza hapo utampata. Baada ya kusikiliza maelezo ya wanachama wa kikundi husika, Msajili ataandaa mkutano ambao huitwa mkutano mkuu wa uanzishaji ambao Msajili mwenyewe ndio atakuwa mwenyekiti wake. Katika mkutano huo itateuliwa kamati ya muda ya uanzishaji ambayo itakuwa na wajumbe 5 – 9 akiwemo katibu, mwekahazina, mwenyekiti na wajumbe wengine.
3. Baada ya kamati ya uanzishaji kuundwa itakuwa na kazi ya kushirikiana na Afisa Ushirika kuandaa katiba za chama, sera, miongozo, miradi ya kiuchumi, taratibu za viingilio na taratibu zote za uanzishaji na uendeshaji.
4. Baada ya kazi hiyo kukamilika basi maombi rasmi ya kuomba kusajiliwa yatawasilishwa kwa huyo Afisa Ushirika wa Wilaya yakiambatana na nakala nne za sera za chama, kidadisi


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 38 1/3/2017 10:32:49 AM

uchumi, makadirio ya mapato na matumizi, mihutasari ya mikutano miwili, na ada kama itakavyoelekezwa na afisa ushirika.

## 4.6 FURSA YA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI

Fursa ya mafunzo ya ujasiriamali kwa kawaida inatolewa na taasisi za kiserikali kama vile SIDO, VETA, taasisi za kidini na binafsi.

### *4.6.1 Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA)*

Hii ni taasisi ya kiserikali inayojishughulisha na utoaji wa mafunzo ya ufundi na kusimamia kanuni na taratibu zote za elimu ya ufundi stadi. Vyuo vya elimu ya ufundi stadi (VETA) viko katika mikoa mbalimbali ya Tanzania na vinatoa mafunzo ya upishi, useremala, saluni, ufundi wa magari, umeme, udereva n.k.

Taratibu za kujisajili kwa ajili ya kozi kwenye chuo chochote cha VETA zinapatikana kwa kuwasiliana kwa moja kwa moja na:

*Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi (VETA)*
*Barabara ya Chang'ombe – Temeke*
*Dar es Salaam*
*Simu namba: +255 22 2863683*
*Barua pepe: info@veta.go.tz*
*Tovuti: www.veta.go.tz*

### *4.6.2 SIDO (Small Industries Development Organization)*

Hii pia ni miongoni mwa taasisi za kiserikali zinazotoa fursa za mafunzo ya ujasiriamali. Lengo la kuanzishwa kwa SIDO ni pamoja na kutoa mafunzo kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda vidogo kwa mtu mmoja mmoja ambaye angependa kujiajiri au kujishughulisha na ajira kwenye viwanda vidogovidogo na kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye masuala ya viwanda vidogo vidogo. Mafunzo yanayotolewa na SIDO ni pamoja na usindikaji wa vyakula, uzalishaji wa ngozi, batiki na jinsi ya kutafuta masoko.

Ofisi za SIDO zinapatikana kwenye mikoa mbalimbali ya Tanzania ikiwemo Tanga, Tabora, Mara, Singida, Shinyanga, Rukwa, Ruvuma, Pwani, Mwanza, Mtwara, Mbeya, Morogoro, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Dodoma, Iringa, Kagera, Arusha na makao makuu ni Dar es Salaam. Mtu yeyote anayehitaji huduma kutoka


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 39 1/3/2017 10:32:50 AM

SIDO anaweza kuwasiliana nao moja kwa moja kwa kufika kwenye ofisi zao.

### 4.6.3 *Taasisi za kidini na binafsi (fursa ya mafunzo kwa ajili ya kuajiriwa na kujiajiri)*

Fursa nyingine za mafunzo ya ujasiriamali zinatolewa na taasisi za kidini na binafsi. Mafunzo yanayotolewa ni pamoja na useremala, uuguzi, ufugaji, upishi, jinsi ya kuanzisha na kuwa na biashara yenye faida na kadhalika.

### 4.6.4 *Maonyesho ya Kibiashara na sikukuu ya Nanenane (Fursa ya kutangaza biashara)*

Wanawake wajasiriamali wanapata fursa ya kutangaza na kuuza biashara zao kwenye maonyesho ya kimataifa ya kibiashara. Mfano wa maonyesho ya kitaifa ya biashara ni yale yanayojulikana kama 'Maonyesho ya Sabasaba' ambayo huratibiwa na Tantrade (Tanzania Trade Authority). Kwa kawaida maonyesho haya hufanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere vilivyopo barabara ya Kilwa wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam kuanzia mwishoni mwa mwezi Juni na kufungwa katikati ya mwezi wa Julai kila mwaka. Kwenye maonesho haya nchi mbalimbali za nje na ndani ya Afika hushiriki katika kuonesha bidhaa zao. Utaratibu wa jinsi ya kushiriki unapatikana kwenye ofisi za Tantrade zilizopo ndani ya viwanja hivyo. Pia taasisi mbalimbali kama PRIDE, EOTF huwaleta wanawake toka sehemu mbalimbali za Tanzania ili waweze kuonyesha bidhaa wanazozitengeneza na kujifunza kutoka kwa wengine.

Maonyesha mengine ni pamoja na maonyesho ya sikukuu ya Nanenane ambayo taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, vikundi vya wanawake wajasiriamali hupata fursa ya kushiriki na kutangaza biashara zao za mazao mfano uzalishaji wa korosho, karanga, asali, uvuvi, ufugaji na kazi za mikono kama vile ususi wa vikapu, shanga, ufinyanzi, usukaji wa mikeka n.k. Ni wajibu wa wanawake kuchangamkia fursa hizi ili kuweza kujikwamua kiuchumi.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 40 1/3/2017 10:32:50 AM

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 HATUA ZA KUJENGA JAMII ISIYOKUWA NA UKATILI WA KIUCHUMI

### 5.1. MABORESHO YA KISERA NA KISHERIA

Katika mijadala iliyotangulia tumetambua uwepo wa juhudi za serikali katika kujenga mikakati ya kutokomeza ukatili wa Kiuchumi. Moja ya juhudi hizo ni pamoja na Mpango wa Taifa wa Kumaliza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto( 2017 - 2022), Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu(2013- 2017) na Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA II). Mipango hii ni mizuri na inahitaji kupatiwa umakini wa kimkakati ili iweze kuwa na matokeo bora.

#### *5.1.2. Sheria ya kimila ya mwaka 1963*

Vifungu vya Sheria vinavyomnyima haki mjane, au kumpa kiwango kidogo urithi mtoto wa kike vinahitaji kufanyiwa marekebisho. Kwa mfano Sheria ya Kimila ya mwaka 1963 inayomnyima mjane kurithi mali za marehemu mume wake, na watoto wa kike kupewa fungu dogo la mali za marehemu baba yao kuliko wanaume. Kuendelea kuwepo kwa vifungu hivi kunanyima haki ya wanawake kumiliki mali na hivyo kuendelea kuwafanya waishi kwenye lindi la umaskini. Aidha, serikali itunge sheria ya mirathi itakayozingatia usawa wa kijinsia, na kukataza ubaguzi wa aina yoyote wakati wa mgawanyo wa mali ya marehemu.



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 41 1/3/2017 10:32:50 AM

### *5.1.3. Sheria ya Ndoa*

Serikali inapaswa kuweka bayana kwenye sheria kwamba iwapo wanandoa wataachana, basi mgawanyo sawa wa mali utolewe na mahakama kwa kila mwanandoa.

Kuna haja ya uwepo wa sheria inayosajili VICOBA ili kuweka mfumo kamili na unaotambulika kisheria.

## 5.2. UHAMASISHAJI JAMII

Uhamasishaji wa jamii wenye kulenga kuchochea mabadiliko ya tabia ni mbinu ya msingi katika kuondoa mitazamo hasi kuhusiana na mila na desturi zilizopitwa na wakati na zizazowakandamiza wanawake mathalan zinazowanyima wanawake haki ya Kiuchumi. Kampeni juu ya kupinga ukatili wa Kiuchumi zifanywe na serikali, taasisi zisizo za kiserikali zikishirikisha jamiii kupitia serikali za mitaa na vijiji ili kuondoa ukatili wa Kiuchumi katika jamii ya Kitanzania. Ushirikishwaji wa jamii utasadia kupiga vita mila na desturi zinazowanyima wanawake kumiliki, kurithi, kutumia mali hususan ardhi ili kujikwamua Kiuchumi. Uhamasishaji huu unaweza kufanyika kwa kutoa elimu, kufanya ushawishi na utetezi wa mabadiliko mbalimbali ya sera na sheria zinazoendeleza ukatili wa Kiuchumi kwa jamii.

## 5.3. WADAU WA MAENDELEO

Wadau wa maendeleo wana wajibu wa kuendelea kuisaidia serikali, Azaki na taasisi mbalimbali  katika kufanikisha utoaji wa elimu juu ya haki za Kiuchumi ili kupinga ukatili na ubaguzi unaofanywa dhidi ya wanawake , watoto wa kike na hata watu wenye ulemavu.


Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 42 1/3/2017 10:32:50 AM

## 5.4. UTAFITI

Ni vyema utafiti wa kina ukafanyika ili kujua ukubwa wa tatizo la ukatili wa Kijinsia wa Kiuchumi kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwa na takwimu na kuweza kupanga mbinu za kulitatua tatizo. Mpaka sasa kwa mfano haijulikani ni wanawake wangapi wanamiliki ardhi, nyumba, walio na hati miliki, idadi ya wanawake walioweza kupata mikopo ya nyumba inayotolewa na taasisi mbalimbali mfano Shirika la Nyumba la Taifa. Kama kuna wanawake wamepata haki miliki au mikopo ya nyumba na ni wanawake wa kada gani?, Je, ni wafanyakazi wa serikali , taasisi binafsi, wajasiriamali wadogo au wakulima?

# HITIMISHO

Mwisho kabisa tunaamini kuwa, kitabu hiki kitakuwa mwongozo na mwanga kwa jamii hususani wanawake katika kujikwamua kiuchumi. Ni imani ya Shirika La WiLDAF kuwa elimu iliyopo katika kitabu hiki itasaidia kupunguza umaskini, kuimarisha usawa wa kijinsia katika swala zima la kumiliki mali na kumaliza kabisa utegemezi wa wanawake hapa nchini na katika jamii hasa za vijijini, hivyo kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia wa kiuchumi.

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho 1**

**A: FOMU YA USAJILI WA BIASHARA YA MTU BINAFSI**

**Fomu 3**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA)**
**BUSINESS NAMES (REGISTRATION) ACT (Cap. 213)**
**(SHERIA YA KUANDIKISHA MAJINA YA BIASHARA) [Sura ya 213]**
**Statement of Particulars by an Individual [Fomu ya Mtu mmoja}**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Business Name to be registered<br>***(Jina la biashara unalopendekeza)*** | | | | |
| 2. | Nature of business*<br>**(Biashara utakayokuwa unafanya)*** | | | | |
| 3. | (a) Postal address<br>***(anwani ya Posta)*** | | | | |
| | (b) Business address<br>***(Mahali ilipo biashara):*** | **Number (Namba)** | **Street (Mtaa)** | **District (Wilaya)** | **Region (Mkoa)** |
| | | | | | |
| | (c) Phone numbers (Namba za simu) | | | | |
| | (d) E-mail (Barua pepe) | | | | |
| 4. | Applicant's full names<br>***(Majina kamili ya Muombaj)*** | | | | |
| 5. | Applicant's Nationality, age and sex<br>***(Uraia, Umri na Jinsia ya mwombaji)*** | **Nationality (Uraia)** | | **Age (Umri)** | **Sex (Jinsia)** |
| 6. | Residential address **(Anwani ya makazi)** | **Number (Namba)** | **Street (Mtaa)** | **District (Wilaya)** | **Region (Mkoa)** |
| 7. | Other Business Occupation **(Unafanya shughuli/kazi gani nyingine?** | | | | |
| 8. | Have you ever used this Business name before? (Je umeshaanza kutumia jina hili la biashara? | (a) YES state the date that you have started using it). **NDIYO (andika tarehe uliyoanza kulitumia)** | | | |
| 9. | | (b) NO (write the date that you are applying) **HAPANA (andika tarehe ya kuletwa ombi hili)** | | | |
| 10. | Application date **(Tarehe ya kuleta ombi hili)** | | | | |
| 11. | Applicant's signature **(Saini ya Muombaji)** | | | | |

***The use of general terms e.g., "wholesale and retail" must be avoided. Particulars sufficient to identify the type of business carried on must be given. (Epuka matumizi ya maneno ya jumla jumla kama vile "Biashara ya jumla" au "Biashara ya rejareja". Elezea kwa ufasaha aina/shughuli ya biashara unayofanya).**

1



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 44 1/3/2017 10:32:51 AM

**Kiambatanisho Na: 3**

**FOMU YA MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA** **TFN 211**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**FOMU YA MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA**

Imetolewa na kifungu cha 11 (1) cha Seria ya leseni za Biashara Na. 25 ya 1972 – Issued under section 11(1) of Business lisecing Act No. 25 of 1972)

(i) Jaza fomu mbili (2) kwa maombi ya leseni kundi "A" NA FOMU MOJA KWA KUNDI 'b" Futa isiyohusika kwenye alama ya nyota (*) Fill in two (20 forms for licences in schedule "A" and one. (1) for schedule "B"

(ii) Maombi yanayorudiwa yapelekwe moja kwa moja kwa Ofisa mtoaji leseni anayehusika (angalia makundi "A" na "B" ukurasa wa 3-4) kwa uamuzi baada ya kujazwa na mwombaji. (Applications for renewal should be sent directly to relevant lincencing officer (see schedule "A" and "B", page 3 and 4)

(iii) Maombi mapya yanayopita ngazi zote za mwanzo (Tazama kifungu 14) ni yale makundi "B" peke (ITEM No. 14 (i) – (ii) applies to new lincences in schedule "B" only)

(iv) Leseni itakayotolewa bila kukamilika ngazi zinazoihusu haitatambuliwa kuwa leseni halali (any licence if issued without undergoing the prescribes procedures illiegal).

(v) Mwombaji atakayetoa maelezo ya uongo atashtakiwa na/au ombi lake kukataliwa (an applicant who give false information may be sued or his application may be rejected).

(vi) Viwango vya ada leseni vitarekebishwa mara kwa mara kulingana na kifungu cha 8(2) cha Sheria ya leseni za BIASHRA Na. 25 ya mwaka 1972. (Licence fee will be reviewed from time to time as per section 8(2) of Act 25 of 1972).

(vii) Maombi ya leseni yasihusishwe au ulipaji wa michango au malipo mengineyo yoyote yasiyohusu sheria hii, isipokuwa ada ya leseni ya biashara, faini au adhabu pale inapohusika chini ya sheria hii (compulsory collection of fees/contributions from applicant other than those prescribed in the schedule to Act. 25 of 1972 and in the current Finance At are illegal).

1. Jina la mwombaji (taja kama ni kampuni, jina la biashara au mtu binafsi (Name of applicant – ca. or natural person) ……………………………..……………
2. Namba ya hati ya kuandikishwa (Reg/Cert. of incorporation)………….………….

2



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 45 1/3/2017 10:32:51 AM

3. Uraia wa mwenye biashara (mwenye hisa) (share holders, citizenship)……………………………………………………………….…………………….

4. Anuani ya postal (Postal address)…………………………………………* mji/kijiji Town/village………………………… simu (telephone)………………………… Fax No: ……………………………………… email…………………………………

5. Wilaya (district)……………………… kata (ward)……………………………….. Mtaa (street)………………………………………………………………………..

6. Namba ya kiwanja cha biashara (business premises), Plot No………… block ………………………… Nyumba Na. (House Na.) ………………………………………………………..

7. Namba ya leseni iliyomalizika (iwapo ni ombi jipya andika (mpya) (No. of previous licence/state if new)…………………… Tarehe ilipotelwa (date of issue) ………………………Tarehe ya mwisho ya kutumia (expiry date)…………………….. ada iliyolipwa (fee paid) …………………………………

8. Namba ya mlipa kodi (taz payer indentification number) – TIN………………………………………

9. Jina la Mkurugenzi au meneja (director's/ manager's name)…………………………………………..

10. Aina ya biashara inayoombwa (Line of business being applied for) ………………………………………………………………………. (Tazama baadhi ya makundi ya aina za biashara kwenye fomu hii uk. 3-4 (see some of business categories/lines in this form page 3-4) kama aina ya leseni unayoomba haipo katika orodha iandike (if the line no listed simply write it).

11. Ikiwa leseni inayoombwa ni kwa ajili ya tawi (branch) la biashara yako basi eleza: state whether it is branch/ subsidiary licence)

(i) Namba ya Leseni yako kuu (No. of Principal licence)………………..

(ii) Ada iliyolipwa (fee paid)…………………………………………………...

12. Umewahi kuhukumiwa kwa kosa lolote la jinai katika miezi kumi na miwili iliyopita? Ndiyo/Hapana. Kama ndiyo eleza kosa (Have you ever been convicted for any criminal offence for the last 12 months? Yes/No. Explain if yes.)

……………………………………………………………………………………………………….

13. Uthibitisho wa mwombaji (Certificate of Applicant)

*Ninathibitisha/tunathibitisha kwamba yote yaliyoelezwa hapa juu iya kweli kama nijuavyo/tujuavyo na niaminivyo/tuaminivyo. (I/We declare that the above information's correct to the best of my knowledge/our knowledge)

Tarehe ya kujaza fomu (date of application)…………………………………

3



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 46 1/3/2017 10:32:52 AM

Saini ya mwombaji au mkurugenzi kwa niaba ya kampuni iliyo "Limited" (Applicant/Director's signature

……………………………………………………………………………………………………

Mhuri (Rubber stamp) ……………………………………………………………

14. Maoni /Uamuzi kuhusu maombi (for official use at village/Land/Health and Licencing Committees).

| | Apewe/Asipewe | Maelezo | Tarehe | Sahihi/Muhuri |
|---|---|---|---|---|
| (i) Serikali ya kijiji (Maombi maya) ya vijijini kundi "B: | | | | |
| (ii) Afisa wa Afya (Maombi yote mapya) ya Hoteli za kawaida. Vilabu vya pombe. Utengenezaji/Uuzaji vyakula na vinywaji | | | | |
| (iii) Afisa biashara (maombi yote) | | | | |
| (iv) Afisa mipnago Miji/Halmashauri ya Wilaya/Manispaa/Jiji. | | | | |
| (v) - Halmashauri ya Wilaya<br>- Manispaa/Jiji<br>- Wizara | | | | |

15. Kwa matumizi ya ofisi tu (for official use only)

Ada iliyolipwa Shs……………………………….. Namba ya Stakabadhi…………… Ya tarehe………………………………………………………. 20……………………..

……………………………………

Sahihi na Muhuri wa Mpokeaji

Namba ya leseni……………………… ya tarehe………………….. 200……………...

…………………………………..

Sahihi ya Muhuri wa Mpokeaji

Tarehe…………………………….. 200…………………………………………………..

4

**MAKUNDI NA AINA ZA BIASHARA – KUNDI "A" (LINE OF BUSINESS SCHEDULE "A")**

Maombi yapelekwe Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo pia itapokea malipo ya ada na kutoa leseni (to be sent to licencing officer / Committee at the ministry of Industry and Trade, which will also collect the licence fees and issue the licence):

1. Umiliki/ ujenzi majengo/Wakala wa mali (Estate Agent, Estate developer, Property Management, Rent Estate Agent)
2. Wakala wa shughuli za meli (Shipping Agency)
3. Uendeshaji wa shughuli za meli (Shipping Business)
4. Commercial traveller.
5. Wakala wa kupokea na usafirishaji mizigo (Cleaning and Forwarding/Freight Fowarders).
6. Bima (Insurance and Assurance, Insurance broker, Re-Insurance)
7. Biashara za kitalii (Tourist hotels, Lodges, Camps, Tour operators, Hunting safaris, Travel Agent, Car hiring or Renting, Tourist photographic and Tourist promotion).
8. Benki na huduma za fedha (Banking and financial institutions, Capital market and Credit card, Management stock exchange and stock exchange brokers).
9. Usafirishaji wa abiria na mizigo kwa ndege (Transportation of passengers or goods by Air)
10. Huduma za posta (Postal service)
11. Usafirishaji abiria na mizigo kwa reli (Transportation of passengers or goods by railway)
12. Huduma za mawasiliano (Fax, E-mail, Internet services provider, Internet café, Internet surfing, Telecommunication services and Sales of Telecommunication Equipments).
13. Uthamini wa mizigo (Cargo valuation, cargo superintendence and pre-shipment inspection)
14. Uhesabu na upangaji wa mizigo melini (Cargo talling)
15. Bandari (Harbors and Cargo handling)
16. Utengenezaji na usambazaji umeme (Electricity production and distribution)
17. Maduka ya kubadilisha fedha (Bureau de change)
18. Kupakia na kupakua mizigo melini (Stevedoring or lighteraje)
19. Wakala wa kusafirisha vifurushi na barua (courier services and mail agent)
20. Vituo vya Redio na Television (Broadcasting and Television)
21. Ship Chandlers/Miscellaneous port services
22. Usafirishaji wa mafuta mazito (Refining crude oil)
23. Klabu za usiku (Night clubs)
24. Uuzaji na usambazaji wa silaha na risasi (Dealers in arms and Ammunition)
25. Uuzaji na usambazaji wa baruti (Dealers in explosives)
26. Huduma ya hifadhi ya jamii (Social security providers)
27. Uuzaji bidhaa nje (Export and Selling)

5



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 48 1/3/2017 10:32:53 AM

28. Uchimbaji na usambazaji  maji (Water drilling and supply)
29. Uuzaji wa vifaa vya utangazaji (Dealers in broadcasting apparatus)
30. Utengenezaji na uuzaji bidhaa (Manufacturing and selling)
31. Ununuaji na uuzaji wa magari (Motor vehicles dealers)
32. Wakala wa ushuru (Commission agent or manufacturer's representatives)
33. Uagizaji wa bidhaa nje ya nchi (Import and selling)
34. Sonara na biashara ya madini (Gold and silver smith and gemstone dealers)
35. Biashara yoyote ambayo haikutajwa yenye sura ya kitaifa au kimataifa au inayoongozwa na sera. (Any business of National or International nature or governed by policy).

KUNDI "B" (SCHEDULE "B")

**Maombi yatapelekwa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/ Jiji ambayo pia itapokea ada na kutoa leseni (to be sent to lincencing  officer to District/town/ municipal or city council who will also collect the lincencing fees and issue the lincence)**

1. Wakala wa bima (insuarance Agent)
2. Mgahawa, Hotel kawaida, nyumba za kulala wageni (restaurants and ordinary hotels and guest houses.
3. Mnada (auctioneer)
4. Kutembeza biashara (itinerant trade)
5. General merchandizing (super markets), department stores etc.)
6. Kampuni za biashara za mikoa (regional trading companies)
7. Vyama vya ushirika (cooperative societies)
8. Uuzaji wa bidhaa za jumla (wholesale trade)
9. Ujenzi wa kandarasi (building contractors, electrical contractors, mechanical contractors, civil works, contractors etc.)
10. Utaalamu ya ushauri wa kitaalamu (specified professionals).
11. Uchapishaji wa vitabu na magazeti (printing and Publishing of books and newspapers).
12. Vipuri (Spare party, machine tools)
13. Udalali (Brokers)
14. Usafirishaji wa abiria mjini ( transportation of passengers within the city, municipality and Township)
15. Viwanda vidogo (small scale manufacturing and selling)
16. Simu za kwenye vibanda (attended telephone services)
17. Biashara yeyote ambayo haikutajwa na haina sura ya kitaifa ua kimataifa na isiyoongozwa na sera (any other business which is not of national/international nature or not governed/processed by policy).

**<u>Kumbuka</u>: Masharti ya kuomba leseni za biashara kwa makundi "A" NA "B" ni kama yalivyoelezewa kwenye kipengele cha utaratibu wa kuomba leseni hapo juu.**

**Kiambatanisho: Na: 3**

LESENI YA BIASHARA

B. 21922788

(Imetolewa chini ya Sheria ya leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972, marekebisho ya mwaka 1980 na masharti yaliyo nyuma)

*Futa isiyotakiwa

1. Ofisi iliyotolewa…………………………………………………………………………………
2. Nambari ya Ushuru wa mapato………………………………………………………….
3. Leseni imetolewa kwa……………………………………………………………………...
   Kuendesha biashara ya…………………………………………………………………………
   Katika wilaya/kanda ya……………………………… mtaa wa…………………………
4. Ni ya shina/tawi…………… Ada Shs…………… nambari ya stakabadhi…………….
   ya tarehe……………………………………………………………………………
5. Mpya inaendeleza* muda wa leseni Na…………………………………………………..

(II) Muda wa leseni hii utaisha tarehe…………………………………………………………...

Tarehe…………………………… ……………………………………………………..

Saini na mhuri wa mtoaji leseni

**Kumbuka:** Leseni hii hapo juu ndizo zinazotolewa na Halmashauri ya Wilaya au Manispaa kwa mfanyabiashara.

7



Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 50 1/3/2017 10:32:54 AM

Fursa na Haki za wanawake Kiuchumi book.indd 51 1/3/2017 10:32:54 AM